**NENO KUTOKA KWA MKUU WA TAASISI YA TEKNOLOJIA DAR ES SALAAM, PROF. PREKSEDIS MARCO NDOMBA, KWA NIABA YA WASHIRIKI WA VYUO NA TAASISI ZA ELIMU YA JUU, KATIKA HAFLA YA KUFUNGA MAONYESHO YA 12 YA VYUO VYA ELIMU YA JUU, SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 29 JULAI, 2017, KATIKA VIWANJA VYA MNAZI MMOJA – DAR ES SALAAM.**

- Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Riziki Pembe (Mb);

- Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Simon Msanjila;

- Makatibu Wakuu na Viongozi Waandamizi wa Serikali mliopo hapa;

- Katibu Mtendaji wa Tume ya Vyuo Vikuu, Prof. Eliuter Mwageni;

- Wakuu wa Vyuo na Taasisi mbalimbali za Elimu mliopo hapa;

- Watendaji Wakuu wa Mashirika mbalimbali mliopo hapa;

- Washiriki wa maonyesho haya kutoka vyuo vya ndani na nje ya nchi;

- Wananchi na wanafunzi watarajiwa wa vyuo vya elimu ya juu mliopo hapa;

- Wageni waalikwa;

- Wanahabari;

- Mabibi na Mabwana;

- Habari za mchana!

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Ninamshukuru sana Mwenyenzi Mungu kwa kupewa fursa hii ya kuwawakilisha Wakuu wa vyuo vya elimu ya juu vya ndani kutoa neno la shukrani kwenye halfa hii ya kufunga maonyesho ya 12 ya vyuo na Taasisi mbalimbali za elimu ya juu.

Kwa niaba ya wakuu wa vyuo walioshiriki katika maonyesho haya, kwa kipee kabisa, ninamshukuru Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa (Mb), kwa kutufungulia maonyesho haya siku ya Jumatano tarehe 26 Julai, 2017. Tumefarijika sana kwa kutenga muda wake adimu kutembelea mabanda mbalimbali ya maonyesho ili kujionea shughuli zinazofanywa na vyuo na taasisi mbalimbali za elimu ya juu.

Aidha, nachukua fursa hii kukushukuru Mgeni wetu rasmi, Mhe. Riziki Pembe, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa kukubali kuungana nasi na kutufungia maonyesho haya.

Kwa heshima za kipekee, napenda kumshukuru Prof. Simon Msanjila, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kushiriki nasi katika hafla hii. Pamoja na shughuli nyingi alizonazo, bado ameweza kutenga muda wa kuwa nasi katika tukio hili muhimu.

Nawashukuru pia waandaaji na waratibu wa maonyesho haya, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), chini ya usimamizi madhubuti wa Prof. Eliuter Mwageni, kwa maandalizi mazuri na yaliyofana, ambayo yamefanya maonyesho haya kuwa ya faida kubwa kwa wadau mbalimbali wa elimu wa ndani na nje ya nchi yetu.

Ninawashukuru pia washiriki wote wa maonyesho haya, hususani wanafunzi watarajiwa waliokuja kujifunza jinsi ya kufanya udahili na

kujifunza shughuli mbalimbali zitolewazo na vyuo vikuu. Bila wao, maonyesho haya yasingefana sana.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Baadhi ya faida zilizopatikana kwenye maonyesho haya ni kama ifuatavyo:

Faida kubwa iliyotokana na maonyesho ni kwamba yamerahisisha mchakato wa udahili wa wanafunzi katika vyuo mbalimbali kwani, kwa kutembelea maonyesho haya, mwanafunzi mtarajiwa amepata fursa ya kutembelea na kupata mahitaji ya udahili ya vyuo zaidi ya kimoja, na hivyo kuwa na uwanda mpana wa kufikiri na hatimaye kuamua ni chuo kipi ajiunge nacho.

Maonyesho haya pia yamefungua fursa za ushirikiano baina ya vyuo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi vilivyoshiriki.

Tumeshuhudia pia ushiriki mkubwa wa wadau wa elimu yakiwemo mashirika ya mifuko ya jamii kama PSPF na PPF.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kama washiriki wa maonyesho haya, tumefurahi kuwa sehemu ya watoa huduma kwa jamii, na pia tumepata fursa ya kutangaza shughuli zetu zikiwemo tafiti na bunifu mbalimbali ambazo ni matokeo ya mafunzo tunayotoa kwa wanafunzi wetu.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Mbali na faida tulizozipata kama taasisi za elimu ya juu, tunayo mapendekezo machache ya jinsi ya kuboresha maonyesho haya kwa siku za usoni ili yawe ya kufana zaidi:

Kwanza, tunaomba muda wa maonyesho haya katika siku zijazo uongezwe na kufikia siku tano hadi saba ili kutoa mwanya zaidi kwa wadau kutembelea na kupata muda wa kutosha kutafakari na kufanya maamuzi makini katika chaguzi za vyuo na taasisi za kujiunga.

Pili, Waandaaji na waratibu wa maonyesho haya ambao ni TCU, waone uwezekano wa kuwashirikisha NACTE katika maandalizi haya ili kuongeza idadi ya vyuo shiriki vya kada mbalimbali za elimu nchini.

Tatu, tunaomba wadau na watoa huduma za jamii wengi zaidi kama vile mashirika, makampuni na taasisi mbalimbali zilete huduma zao wakati wa maonyesho kama ilivyofanywa na ndugu zetu wa PPF , PSPF na wengine.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kama vyuo vya elimu ya juu, tumegushwa sana na hotuba ya ufunguzi ya Mhe. Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, iliyotutaka tuboreshe mafunzo tunayotoa kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu ili yaweze kuwasaidia wahitimu kujiajiri na kuchangia katika maendeleo ya uchumi wa viwanda.

Mwisho kabisa, kwa niaba ya washiriki wote, nikuhakikishie kuwa tutaendelea kuboresha mitaala ya mafunzo na kusimamia utoaji bora wa mafunzo, tafiti na huduma za jamii ili kuinua hali ya uchumi wa taifa letu na hatimaye kuwa mabalozi wazuri wa kutangaza na kusimamia maendeleo ya nchi yetu ambayo yatatufikisha katika uchumi wa kati wa viwanda.

**Asanteni kwa kunisikiliza.**